# SHERIA YA KUANZISHA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

**VIFUNGU** **MAELEZO**


## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

1. Jina fupi na Kuanza Kutumika.
2. Ufafanuzi.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA NA KAZI ZA HOSPITALI

3. Kuanzishwa kwa Hospitali.
4. Kazi za Hospitali.

## SEHEMU YA TATU
## UONGOZI WA HOSPITALI

5. Kuanzishwa kwa Bodi.
6. Muda wa Bodi.
7. Kusita kuwa Mjumbe.
8. Kazi za Bodi.
9. Vikao vya Bodi.
10. Akidi ya Vikao.
11. Utaratibu wa Bodi.
12. Posho.
13. Kumbukumbu za Vikao.

## SEHEMU YA NNE
## MKURUGENZI MTENDAJI NA WAFANYAKAZI

14. Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.
15. Sifa za Mkurugenzi Mtendaji.
16. Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji.
17. Kuanzishwa kwa Idara.
18. Uteuzi wa Wakurugenzi wa Idara.
19. Kamati ya Uongozi.
20. Majukumu na Kazi za Kamati ya Uongozi.
21. Wafanyakazi wengine..

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

22. Fedha za Hospitali.
23. Kubakiza fedha.
24. Kutumika kwa Sheria ya Fedha za Umma.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MBALIMBALI

25. Kinga.
26. Kuhaulisha mali na madeni.
27. Huduma bila ya malipo.
28. Kanuni.

**SHERIA NAM. 3 2016**
**NIMESAINI**

{**DR. ALI MOHAMED SHEIN**}
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**

25th July 2016

# SHERIA YA KUANZISHA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar

---

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ya 2016 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataitangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Ufafanuzi.

**2.** Katika sheria hii isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"Bodi"maana yake ni Bodi ya Hospitali iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria hii;

"Idara" maana yake ni Idara iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 17 cha Sheria hii;

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu cha 15 (1) cha Sheria hii;

"Hospitali" maana yake ni Hospitali ya Mnazi Mmoja iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na mambo ya afya;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA NA KAZI ZA HOSPITALI

Kazi za Hospitali.

**3.**-(1) Kunaanzishwa Hospitali itakayojulikana kama Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo itakuwa ni Wakala wa Serikali.

(2) Hospitali itatekeleza kazi zake kwa ushauri wa Bodi na usimamizi wa Waziri.

Kuanzishwa kwa Hospitali

**4.**-(1) Kazi za Hospitali zitakuwa:

(a) kutoa huduma kama Hospitali ya Rufaa na kuweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya;

(b) kutekeleza majukumu ya udhibiti na usimamizi wa Hospitali nyengine yoyote kama ilivyopewa chini ya Sheria hii au Sheria nyengine yoyote;

(c) kuwahudumia wagonjwa wa nje na wa ndani kwa mujibu wa maadili ya kinga na tiba ;

(d) kushajihisha na kuendeleza mipango ya uwezeshaji na uendelezaji wa afya na ustawi kwa ujumla kwa watu wa Zanzibar;

(e) kusaidia Serikali na jumuiya nyengine au taasisi katika kupanga, kutekeleza, kufanya mapitio na marudio ya mpango wa elimu ya afya kwa manufaa ya umma;

(f) kuandaa na kusimamia Hospitali kuwa kama mshauri mwelekezi wa kitaifa na kuwa Hospitali ya kufundishia;

(g) kutoa huduma za kawaida zinazotolewa na mshauri mwelekezi na Hospitali ya kufundishia;

(h) kutoa huduma kwa ajili ya sehemu na vituo vya kujifunzia, mafunzo na utafiti katika taaluma za sayansi ya afya na masomo mengine yoyote yanayohusiana na hayo kama itakavyoamuliwa na Bodi muda hadi muda;

(i) kuweka mazingira mazuri na kusaidia mafunzo ya wafanyakazi wa afya kwa Hospitali na yanayohusiana na sayansi au taasisi nyengine zozote zinazotoa mafunzo ya afya;

(j) kutoa ushauri, ushauri elekezi na huduma nyengine kwa Serikali, Mashirika na kwa watu binafsi kwa msingi wa maendeleo ya huduma za matibabu na huduma za afya, na ustawi mzuri wa watu kwa ujumla ndani ya Zanzibar;

(k) kutekeleza, ama peke yake au kwa kushirikiana na mtu mwengine yeyote au mashirika ndani au nje ya Zanzibar, kukuza au kuzalisha dawa, vifaa na zana tiba;

(l) kutoa huduma za uchunguzi na huduma zinazohusiana na matengenezo na utunzaji wa Hospitali na vifaa vya maabara;

(m) kusaidia Serikali na taasisi nyengine za umma kuandaa na kuchukua vipimo vinavyohusiana na uhakikishaji wa viwango vya huduma za afya;

(n) kusimamia na kudhibiti kinga na tiba kwa maradhi ya mripuko kwa umuhimu wa afya kwa jamii;

(o) kufanya kazi nyengine kama ilivyopewa Hospitali na sheria nyengine;

(p) kushirikiana na vyuo vilivyoanzishwa ndani ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na chuo chengine chochote kinachotambulika kutoa elimu na mafunzo na kufanya utafiti wa dawa, matibabu ya afya ya binadamu na taaluma za sayansi ya afya na taaluma saidizi na tegemezi;

(q) kuendesha, kujenga, kuandaa, kutunza, kuhifadhi na kufanya matengenezo mali zake;

(r) kuanzisha na kuendeleza uhusiano na vyombo vya ndani, kitaifa, kikanda na kimataifa vinavyojihusisha na utoaji wa huduma za afya na zinazofanana na hizo; na

(s) kufanya kazi nyengine zozote ambazo Bodi itaona ni muhimu.

(2) Katika kutekeleza majukumu yake, Hospitali inaweza kuingia kwenye mikataba na Hospitali nyengine, vyuo, taasisi za sayansi ya afya kwa kuandaa mafunzo na shughuli za utafiti na kuziunganisha na kazi za Hospitali.

## SEHEMU YA TATU
## UONGOZI WA HOSPITALI

Kuanzishwa kwa Bodi.

**5.**-(1) Kunaanzishwa Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Ushauri ya Hospitali ambayo itakuwa na jukumu la kufanya kazi kama chombo cha ushauri kwa uongozi wa Hospitali.

(2) Bodi itaundwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali;

(c) Mkurugenzi Mkuu wa Wizara;

(d) Mwakilishi kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar mwenye taaluma ya sayansi ya afya;

(e) Wawakilishi wawili kutoka sekta binafsi; na

(f) Mwakilishi kutoka Jumuiya ya Kitaalamu ya Afya;

(3) Isipokuwa wajumbe wanaoteuliwa kwa nafasi zao, Wajumbe

wengine wa Bodi watateuliwa na Waziri baada ya kushauriana na taasisi husika.

(4) Wajumbe wa Bodi watateuwa Mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamo Mwenyekiti.

(5) Mwanasheria wa Serikali kutoka Wizara inayohusika na masuala ya Afya atakuwa Katibu wa Bodi.

Muda wa Bodi.

**6.** Wajumbe wa Bodi, isipokuwa wajumbe walioteuliwa kwa nafasi zao, watashika madaraka yao kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya kuteuliwa na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja, isipokuwa kama uteuzi wao utafutwa kabla au utasita kwa sababu nyengine yoyote iliyoelezwa katika Sheria hii.

Kusita kuwa Mjumbe.

**7.** Mjumbe wa Bodi atasita kuwa mjumbe iwapo:

(a) atashindwa kutekeleza majukumu yake;

(b) ametenda kosa kinyume na maadili au kuwa na tabia isiyokubalika na jamii;

(c) amehukumiwa kwa kosa la jinai linalojumuisha udanganyifu au kutokuwa muaminifu;

(d) atashindwa kutangaza maslahi binafsi katika hoja iliyojadiliwa katika kikao;

(e) atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya ruhusa ya Mwenyekiti;

(f) atajiuzulu kwa kutoa taarifa kwa mamlaka ya uteuzi na kueleza sababu za kujiuzulu kwake; au

(g) atafariki.

Kazi za Bodi.

**8.** Bodi itatekeleza kazi zifuatazo:

(a) kushauri juu ya uteuzi, kuweka masharti na vigezo vya utumishi, usitishaji wa utumishi na uteuzi wa maafisa waandamizi ikiwajumuisha wakuu wa idara na wafanyakazi wengine wa Hospitali kadri itakavyoona inafaa;

(b) kushauri juu ya uanzishaji wa Idara na vitengo vyengine kama itakavyoona inafaa;

(c) kupendekeza sera, mpango mkakati, mpango wa usimamizi wa mwaka na kufanya mapitio ya mipango ya utekelezaji;

(d) kuangalia na kusimamia utendaji kazi;

(e) kuhakikisha mazingira mazuri ya fedha ya Hospitali;

(f) kuhakikisha huduma za afya zinazotolewa na Hospitali zikizingatia vipaumbele vya kuhudumia wananchi na kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa uhakika;

(g) kuhakikisha kuwa Hospitali inatekeleza mahitaji ya ufundishaji na utafiti wa huduma za afya na masomo mengineyo ya sayansi yanayoendana na hayo;

(h) kuhakikisha kuwa Hospitali inatekeleza wajibu wake kwa Wizara yenye dhamana ya Afya;

(i) kupendekeza masharti ya utoaji wa huduma na maslahi ya ajira kwa wafanyakazi wa Hospitali kwa kufuata Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria nyengine;

(j) kupendekeza juu ya Sera za fedha za Hospitali, makisio ya matumizi ya mwaka yaliyowasilishwa na uongozi, kusimamia na kufanya mapitio ya taarifa ya fedha na matumizi kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma;

(k) kutoa muongozo na ushauri juu ya uendeshaji wa Hospitali;

(l) kupendekeza utungwaji wa Kanuni za huduma za Hospitali;

(m) kusimamia na kukuza viwango na ubora wa utowaji wa huduma za Hospitali kwa kuzingatia ustawi wa matarajio ya wagonjwa na kukuza miiko na maadili ya kila kada ya afya;

(n) kuanzisha Kamati ambazo zinaonekana ni muhimu katika kukamilisha majukumu;

(o) kupendekeza kwa Waziri juu ya posho ya vikao vya Bodi na Kamati zake; na

(p) kutekeleza jambo lolote ambalo ni muhimu katika utekelezaji wa kazi zake au kama ilivyoelekezwa na Waziri au Sheria hii.

Vikao vya Bodi.

**9.**-(1) Mwenyekiti ataongoza vikao vya Bodi na endapo Mwenyekiti hayupo, Makamo Mwenyekiti ataongoza vikao na endapo Makamo Mwenyekiti hayupo, wajumbe waliohudhuria watamteua mjumbe mmoja miongoni mwao kuongoza vikao vya Bodi.

(2) Bodi itakutana angalau mara moja kwa kila baada ya miezi mitatu kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake na endapo itatokea dharura, Bodi inaweza kukutana wakati wowote.

(3) Mwenyekiti anaweza kuitisha kikao cha dharura wakati wowote baada ya kupokea maombi ya maandishi ya wajumbe walio wengi lakini vikao hivi havitozidi idadi ya vikao vya kawaida.

(4) Maamuzi ya vikao vya Bodi yataamuliwa kwa wingi wa kura za Wajumbe waliohudhuria na kupiga kura, na endapo itatokea kura za wajumbe kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya maamuzi.

Akidi ya Vikao.

**10.** Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wataunda akidi ya vikao vya Bodi.

Utaratibu wa Bodi.

**11.** Bodi inaweza kuweka utaratibu wa kuendesha vikao vyake.

Posho.

**12.** Wajumbe wa Bodi watapaswa kulipwa posho kwa kadri itakavyoamuliwa na Waziri.

Kumbukumbu za Vikao.

**13.** Katibu atanakili na kuweka kumbukumbu zote za vikao vya Bodi, ambazo zitasomwa na kuthibitishwa katika kikao kinachofuata na zitasainiwa na Mwenyekiti na Katibu.

## SEHEMU YA NNE
## MKURUGENZI MTENDAJI NA WAFANYAKAZI

Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

**14.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Hospitali na atawajibika kwa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Hospitali.

Sifa za Mkurugenzi Mtendaji.

**15.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) mwenye taaluma angalau ya shahada ya pili ya tiba, afya ya jamii au uongozi kutoka katika Chuo kinachotambulika;

(c) mwenye uzoefu usiopungua angalau miaka kumi; na

(d) mwenye kiwango kikubwa cha uweledi katika kutekeleza kwa ufanisi na ubora mambo ya Hospitali.

Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji.

**16.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuongoza mambo ya Hospitali na kutoa huduma bora na zinazojitosheleza;

(b) kusimamia mapato na matumizi yanayotolewa na Hospitali kwa mujibu wa Sheria zinazohusika.

(c) kusimamia na kuendeleza utendaji wa majukumu yote ya Hospital ikijumuisha;

(i) uongozi na usimamizi wa kila siku wa Hospitali;

(ii) usimamizi wa fedha, mali na shughuli nyengine za Hospitali;

(d) kutoa taarifa za Hospitali kwa Bodi; na

(e) kufanya kazi au kutekeleza majukumu mengine yoyote aliyopewa na Waziri chini ya masharti ya Sheria hii.

(2) Mkurugenzi Mtendaji anaweza kukasimu majukumu yake kwa mkurugenzi au afisa mwandamizi wa Hospitali.

Kuanzishwa kwa Idara.

**17.**-(1) Kunaanzishwa Idara za Hospitali ambazo zitakuwa kama ifuatavyo:

(a) Idara ya Huduma na Tiba;

(b) Idara ya Mafunzo na Tafiti;

(c) Idara ya Utawala, Rasilimali Watu na Fedha;

(d) Idara ya Dawa na Vifaa Tiba;

(e) Idara ya Ufundi; na

(f) Idara ya Huduma za Uchunguzi wa Afya na Maradhi.

(2) Hospitali inaweza kuanzisha Idara nyengine au kitengo kwa kadri itakavyoona inafaa.

Uteuzi wa Wakurugenzi wa Idara.

**18.**-(1) Bodi inaweza, baada ya kupendekezwa na Mkurugenzi Mtendaji, kuteua wakurugenzi wa Idara kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Wakurugenzi watawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji katika utekelezaji wa majukumu yao.

(3) Mkurugenzi aliyeteuliwa chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atatekeleza kazi za idara yake ikijumuisha kusaidia na kusimamia idara yake.

Kamati ya Uongozi.

**19.**-(1) Kutakuwa na Kamati itakayojulikana kama Kamati ya Uongozi wa Hospitali.

(2) Kamati ya Uongozi itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mkurugenzi Mtendaji ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Wakurugenzi wa Idara;

(c) Mhasibu Mkuu;

(d) Mkaguzi wa Ndani wa hesabu; na

(e) Muuguzi Mkuu wa Hospitali.

(3) Mwanasheria wa Hospitali atakuwa Katibu wa Kamati.

Majukumu na Kazi za Kamati ya Uongozi.

**20.** Kamati ya Uongozi wa Hospitali itakuwa na majukumu na kazi zifuatazo:

(a) kumsaidia Mkurugenzi Mtendaji katika kutekeleza kazi na majukumu yake kwa kuhakikisha sera, mipango na maamuzi ya Bodi yanatekelezwa;

(b) kutoa utaalamu na uongozi wa uwajibikaji kwa madhumuni ya kufikia malengo na makusudio ya Hospitali;

(c) kusimamia uongozi na kutoa huduma za Hospitali zenye kuendana na taratibu na ubora wa Hospitali na sera za Wizara;

(d) kusaidia na kusimamia wakuu wa vitengo kwa kuhakikisha kuwa na uwezo wa kuongoza vitengo vyao na wanawajibika katika kutekeleza majukumu ya vitengo vyao;

(e) kuhakikisha kuwa kuna usimamizi mzuri wa fedha ikiwemo utayarishaji wa bajeti za idara na maamuzi ya matumizi yaliyopitishwa katika bajeti;

(f) kutayarisha na kushauri mipango, sera au miongozo itakayozingatiwa na Bodi;

(g) kushauri juu ya uajiri wa wafanyakazi kwa kushirikiana na wakuu wa vitengo na kupendekeza muundo kwa ajili ya kuidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji na kuuwasilisha kwa Bodi;

(h) kupendekeza kwa Mkurugenzi Mtendaji juu ya mambo yanayohusiana na utendaji wa kazi na shughuli za Hospitali; na

(i) kufanya kazi nyengine kama itakavyokasimiwa na Mkurugenzi Mtendaji chini ya Sheria hii.

Wafanyakazi wengine.

**21.**-(1) Hospitali inaweza, kwa mujibu wa masharti na vigezo, kuajiri au kuteua mfanyakazi au huduma ya mshauri elekezi au mtaalamu kama itakavyoona inafaa kwa utekelezaji mzuri wa majukumu ya Hospitali.

(2) Uajiri wa wafanyakazi wa Hospitali, wataalamu na wasaidizi utafanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

(3) Mfanyakazi anayefanyakazi Hospitali kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, ataendelea kufanya kazi na atachukuliwa kuwa ni mfanyakazi wa Hospitali aliyeajiriwa chini ya masharti ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Hospitali.

**22.** Kutakuwa na Fedha na Rasilimali za Hospitali ambazo zitajumuisha:

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa njia ya ruzuku;

(b) michango, ada, malipo na mikopo ambayo Hospitali inaweza kupokea mara kwa mara kutoka kwa mtu au taasisi yoyote; na

(c) fedha nyenginezo ambazo zitawekwa au kupatikana katika utekelezaji wa kazi au vyenginevyo.

Kubakiza fedha

**23.** Hospitali inaweza kubakiza kiwango cha fedha kilichopatikana kutokana na malipo ya huduma ilizozitoa, kwa kiwango kitakachokubaliwa na Waziri mwenye dhamana na mambo ya fedha.

Kutumika kwa Sheria ya Fedha za Umma.

**24.** Sheria ya Fedha za Umma na sheria nyengine zinazohusiana na mambo ya fedha za Umma, zitatumika kwa mambo yote ya fedha za Hospitali.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MBALIMBALI

Kinga.

**25.** Mjumbe wa Bodi, mfanyakazi au mtu mwengine yeyote ambaye anatoa huduma Hospitali, hatoweza kuwajibishwa binafsi kwa kitendo, jambo au chochote alichokifanya au kuacha kufanya, ikiwa alikifanya kwa nia njema wakati wa utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

Kuhaulisha mali na madeni.

**26.** Mali na madeni ambayo yalikuwa chini ya Hospitali kabla ya kuanza kwa Sheria hii, yatakuwa yapo chini ya Hospitali ikijumuisha faida, dhima, kodi, majukumu na amana za mali, mara baada ya kuanza kutumika Sheria hii.

Huduma bila ya malipo.

**27.**-(1) Hospitali itaendelea kutoa huduma ya afya kwa wagonjwa bila ya malipo kwa kufuata sera na miongozo ya Wizara.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mtendaji anaweza, baada ya kushauriana na kukubaliana na Waziri, kuweka utaratibu wa mgonjwa kuchangia kwa baadhi ya huduma za afya zinazotolewa na Hospitali.

Kanuni.

**28.**-(1) Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga Kanuni juu ya mambo ikijumuisha:

(a) taratibu za ukuzaji wa afya na ustawi wa jumla wa watu;

(b) taratibu za huduma za mafunzo ya Hospitali;

(c) masharti ya sehemu na vituo vya kusomea, mafunzo, na utafiti juu ya sayansi ya afya ikijumuisha anatomia, patholojia na masomo mengine yanayofanana na hayo; na

(d) taratibu za utoaji wa huduma ya upimaji na huduma zinazofanana nazo.

**Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi, tarehe 29 Juni, 2016.**

**RAYA ISSA MSELLEM**
**KATIBU, BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**